# HALMASHAURI YA WILAYA YA IRINGA

## TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA ILANI YA CHAMA CHA MAPINDUZI YA MWAKA 2020 – 2025 KWA KIPINDI CHA JANUARI 2021-JUNI 2021

## UTANGULIZI

Mpango wa utekelezaji wa ilani ya uchaguzi Mkuu ya CCM kipindi cha Januari – Juni 2021 ambao unaarifu juu ya utekelezaji wa shughuli mbalimbali za kiuchumi na kijamii kwa kipindi cha Januari hadi Juni 2021. Mpango huu unagusa sekta muhimu za Kilimo umwagiliaji na ushirika, Mifugo na uvuvi, Viwanda na biashara, Ardhi na maliasili, Elimu ya msingi, elimu ya Sekondari, Afya, Maendeleo ya jamii, na utawala bora ambapo ujenzi wa miundombinu mbalimbali ya umwagiliaji, maghala, mabirika, madarasa, maabara, Mabweni, Zahanati, vituo vya afya, mawodi ya wanaume, wanawake na watoto, Matundu ya vyoo na ununuzi wa madawati umefanyika.
Katika kuteleza mpango huu katika kipindi hicho Jumla ya Tsh 4,642,758,198.07/**=** zitatumika katika kutekeleza shughuli na miradi mbalimbali katika sekta tajwa hapo juu. Mpango huu unatokana na malengo na maelezo ya Ilani yaliyopo katika Ilani ya Chama cha Mapinduzi y a mwaka 2020. Shughuli zilizotekelezwa katika mpango wa ilani wa mwaka 2021 zimeoneshwa katika majedwali hapa chini:-

### SEKTA YA KILIMO, UMWAGILIAJI NA USHIRIKA

| NA | SEKTA/SERA | IBARA | MALENGO/ MAELEKEZO YA ILANI | MPANGO WA MWAKA | UTEKELEZAJI | GHARAMA | MAELEZO |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 2. | SEKTA ZA UZALISHAJI MALI:<br><br>Kilimo cha kisasa ndio msingi katika kujenga uchumi na kina nafasi ya kimkakati katika kukuza ustawi wa | 33 | Kutumia uongozi shirikishi katika kusimamia kilimo na kuwafikishia wakulima vijijini maarifa yanayohusu kanuni za kilimo bora cha mazao wanayolima. | Kutoa mafunzo kwa wanavikundi 4,460 vya wakulima juu ya kanuni za kilimo bora cha mazao ya chakula na biashara katika vijiji 134 kwa kupitia mashamba darasa 423 ifikapo Desemba 2021 | Mafunzo ya kilimo bora yametolewa kwa wakulima 4,521 kupitia mashamba darasa 412 katika vijiji 113 | 3,500,000 | Kazi inaendelea na utekelezaji kwa ushirikiano kati ya Halmashauri na ASDP II kupitia wadau mbalimbali wa kilimo |

| | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Taifa. | | Kuongeza upatikanaji na utumiaji wa pembejeo za kilimo, hususan mbolea, mbegu na miche bora na kuweka mfumo utakaohakikisha upatikanaji wa pembejeo hizo kwa wakulima. | Kuandaa mahitaji ya pembejeo na kusimamia ugawaji wa pembejeo kwa kutumia wauza pembejeo katika vijiji 134 ifikapo Desemba 2021 | Usimamizi wa usambazaji wa pembejeo umefanyika, kiasi cha tani 9,322 za mbolea, tani 3,309 za mbegu zimesambazwa kwa wakulima, tani 2218 za viuakuvu, lita 6421 za viuadudu lita 9273 za viuagugu zimesambazwa kwa kwa msimu wa kilimo 20/21 | 750,000 | Kazi hii imetekelezwa na Halmashauri na ASDP II kupitia wadau mbalimbali wa kilimo |
| | | | | Kutoa mafunzo ya namna bora ya matumizi ya pembejeo kwa wakulima 61,345 ifikapo Desemba 2021 | Mafunzo ya matumizi bora ya pembejeo yametolewa kwa wakulima wapatao 56,273 | 4,000,000 | Kazi hii imetekelezwa na Halmashauri na ASDP II kupitia wadau mbalimbali wa kilimo |
| | | | | Kuongeza idadi ya wauza pembejeo za kilimo kutoka 43 hadi 52 vijijini na kuwapa elimu ya utunzaji na usambazaji wa | Jumla ya wauza pembejeo 9 wameongezeka kwa kipindi cha januari-June na kufanya idadi | 350,000 | Kazi hii imetekelezwa na Halmashauri na ASDP II kupitia wadau mbalimbali wa kilimo |

| | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | pembejeo za kilimo | ya wauza pembejeo kufikia 52 | | |
| | | | | Kuwawezesha wakulima 23 Kuzalisha mbegu za kuazimia ubora (QDS) pamoja na kahawa vikonyo ifikapo Desemba 2021. | Wakulima 23 wamewezeshwa kuzalisha mbegu za kuazimia ubora za mazao ya alizeti na soya. Tani 18.4 za mbegu zinatarajiwa kupatikana. | 2,000,000 | Kazi hii imetekelezwa na Halmashauri na ASDP II kupitia Shirika la Clinton Foundation |
| | | | Kuongeza upatikanaji na matumizi ya zana za kilimo kwa kuishirikisha sekta binafsi, kuhamasisha na kuwezesha vikundi vya wakulima, hususan vijana kupata mikopo ya pembejeo na zana za kilimo kutoka kwenye Mfuko wa Pembejeo. | Kuhamasisha vikundi vya wakulima 12 Kununua matrekta ya mkono (Power tillers) 12 Na matrekta makubwa 8 ifikapo Desemba 2021 | Powertiller 1 imenunuliwa kwa ajili ya kikundi cha Upendo kilichopo Magombwe Skimu ya Mlenge | 2,000,000 | Kazi hii imetekelezwa na Halmashauri na ASDP II kupitia wadau mbalimbali wa kilimo pamoja na wakulima |
| | | | | Kuongeza idadi ya wakulima wanaotumia zana zinazokokotwa na wanyamakazi toka 186,000 hadi 372,000 ifikapo Desemba 2021 | Wadau wamewezesha ununuzi wa ox-plough 8 na mikokkoteni 6 wadau wlionunua ni INADES Formation Tanzania na CARITAS | 1,500,000 | Kazi hii imetekelezwa na Halmashauri na ASDP II kupitia wadau mbalimbali wa kilimo |

| | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | Kutoa elimu ya matumizi ya zana bora za kilimo kwa vikundi 26 vya wakulima ifikapo Desemba 2021 | Elimu ya matumizi ya Paddy Thresher na Reaper imeweza kutolewa katika vikundi 43 katika Skimu za Powaga na Idodi | 500,000 | Kazi hii imetekelezwa na Halmashauri na ASDP II kupitia wadau mbalimbali wa kilimo |
| | | | | Kusimamia usambazaji wa mbegu bora kwa wakulima 81,036 ifikapo Desemba 2021 | Wakulima 11,250 walipatiwa mbegu bora za mahindi na nyanya katika kata 9 na vijiji 30 | 1,000,000 | Kazi hii imetekelezwa na Halmashauri na ASDP II kupitia wadau wa Bayer Tanzania |
| | | | Kuhamasisha uzalishaji wa mazao ya kilimo ya aina zote, hususan mazao makuu ya biashara, mazao ya chakula, mboga na matunda, mbegu za mafuta na muhogo ili mavuno makubwa ya kila zao | Kuongeza uzalishaji wa zao la mahindi kutoka tani 340259.3 hadi tani 400,305 Zao la Tumbaku kutoka tani 160.42 Hadi tani 320.84, alizeti kutoka tani 26,993.1 hadi tani 32,800. Mpunga kutoka tani 85,005.28 hadi tani 102,416,Maharage kutoka tani 27,516.6 hadi tani 36,688.8 Viazi mviringo kutoka tani 35,733.6 | Uhamasishaji wa mazao ya chakula na biashara umefanyika na matarajio ni kuvuna tani 623,238 za mazao ya chakula na Tani 81,655 za mazao biashara. | 2,500,000 | Kazi hii imetekelezwa na Halmashauri na ASDP II kupitia wadau mbalimbali wa kilimo |

| | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | yapatikane ifikapo<br><br>Mwaka 2025 kwa viwango vinavyopimika. | hadi tani 36,216, Parachihci kutoka tani 139.3 hadi tani 153, Pamba kutoka tani 8 hadi 15, Korosho kutoka tani 9.8 hadi 13.5,Soya kutoka tani 350.61 hadi tani 400, Ufuta kutoka tani 73.1 hadi tani 100 ifikapo Desemba 2021 | | | |
| | | | Kuweka msukumo mkubwa wa kilimo cha umwagiliaji maji katika maeneo stahiki ili kuhakikisha kwamba ifikapo mwaka 2025 karibu asilimia 25 ya mahitaji yetu ya chakula inapatikana kwa njia ya kilimo hicho. | Kuongeza miradi ya umwagiliaji kutoka hekta 19,731.9 hadi 23,215 na kuongeza skimu za umwagiliaji kutoka 23 hadi 35 ifikapo Desemba 2021 | Jumla ya hekta 167 za umwagiliaji zimeongezaka baada ya ukarabati wa skimu ya Umwagiliaji Mafuruto kufanyika. ,udhibiti wa banio la asili skimu ya Mkombozi na kurudisha mto kwenye njia yake ya asili katika skimu ya Magozi | 219,000,000 | Shughuli zimetelezwa kwa ufadhili wa serikali ya Japan kupitia JICA hususani mfuko wa FACF na Mapato ya ndani ya Halmashauri |
| | | | | Kufanya usanifu na upembuzi yakinifu wa miradi 2 ya | -Uchunguzi wa awali (base line study) kwa ajili | 5,000,000 | Shughuli hizi zinaendelea na utekelezaji kwa |

| | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | umwagiliaji ifikapo Desemba 2021. | ya maandalizi ya upembuzi yakinifu (feasibility study ) umefanyika katika Skimu za Mkombozi, Magozi na Mlenge | | kushirikiana na Wizara ya kilimo,Tume ya Taifa ya Umwagiliaji, Halmashauri ya Wilaya na ASDP II kupitia wadau mbalimbali |
| | | | | Kuhamasisha na kutoa elimu kwa wananchi juu ya kilimo cha umwagiliaji katika vijiji 5 ifikapo Desemba 2021 | Elimu ya matumizi sahihi ya maji na miundombinu ya umwagiliaji imetolewa katika vijiji 3 ambavyo ni Kiwere, Lugamga, Mlambalasi na Cherehani mkoga | 2,700,000 | Kazi inaendelea kufanyika na Halmashauri kwa kushirikiana na Tume ya Taifa ya Umagiliaaji |
| | | | | Kuongeza vitendea kazi (Usafiri - Pikipiki) kwa maafisa ugani kutoka 8 hadi 13 ifikapo Desemba 2021 | Jumla ya wataalamu wa ugani 10 wamepatiwa usafiri –pikipiki ili kuongeza ufanisi wa utendaji wa kazi | 25,000,000 | Kazi imetekelezwa kwa ushikiano wa FAO TANZANIA na CUAMM na Halmashauri |
| | | | Kuimarisha huduma za udhibiti wa | Kutoa mafunzo na maelekezo rejea kwa wataalam wa ugani | Wataalamu wapatao 56 wamepatiwa | 1,000,000 | Kazi imetekelezwa kwa ushirikiano |

| | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | visumbufu na magonjwa ya mimea kwa kujenga uwezo wa kudhibiti visumbufu vya mazao mara vinapojitokeza ili kumwezesha mkulima kupunguza upotevu wa mazao kabla na baada ya mavuno. | 80 ili kuboresha utaalam ifikapo Desemba 2021 | mafunzo rejea kupitia mradi wa CARE na World Vision | | wa Halmashauri na ASDP II kupitia wadau mbalimbali wa kilimo |
| | | | | Kuendesha kampeni za uelewa kwa vijiji 94 juu ya kuelewa na kutambua dalili za visumbufu vya magonjwa ya mimea ifikapo Desemba 2021. | Mafunzo ya utambuzi, utoaji taarifa na udhibiti wa visumbufu vya magonjwa ya mimea yametolewa katika vijiji 39, jumla ya wakulima 2,126 wamepatiwa mafunzo | 2,800,000 | Kazi hii imetekelezwa na Halmashauri na ASDP II kupitia wadau mbalimbali wa kilimo |
| | | | | Kutoa elimu ya kupunguza upotevu wa mazao kabla na baada ya mavuno kwa wakulima 61, 235 katika vijiji 134 ifikapo Desemba 2021 | Wakulima 21,270 katika Tarafa za Pawaga, Idodi, Kiponzelo na Mlolo wamepatiwa elimu ya kukabiliana na upotevu wa mazao wakati na baada ya mavuno | 900,000 | Kazi hii inaendelea kutekelezwa na Halmashauri pamoja na ASDP II kupitia wadau mbalimbali wa kilimo |

| | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | Kuhamasisha ujenzi na matumizi ya maghala bora ya kuhifadhia mazao na kutoa mafunzo juu ya teknolojia sahihi za hifadhi bora kwa lengo la kupunguza upotevu wa chakula. Mpango mkakati uandaliwe wa kupanua hifadhi ya mazao ya chakula katika maeneo ya nchi ambako mazao ya chakula yanalimwa kwa wingi | Kuhamasisha matumizi ya maghala 8 ya hifadhi ya chakula yaliyoko katika vijiji 8 ifikapo Desemba 2021 | Ghala moja la Isele limeanza kuhifadhi Mpunga hivyo wakulima wameanza kuweka Nafaka ghalani mpaka sasa hivi wameweka STEKI MOJA | 5,000,000 | Kazi hii imetekelezwa na Halmashauri na ASDP II kupitia wadau mbalimbali wa kilimo |
| | | | | Kutoa mafunzo juu ya kuanzisha mfumo wa stakabadhi ghalani kwa wakulima 360 katika vijiji 6 ifikapo Desemba 2021 | Elimu imetolewa kwa wakulima 256 katika vijiji vya Isele, Luganga, Idodi na Tungamalenga | 1,155,500 | Utekelezaji unaendelea kwa ushirikiano wa Halmashauri na ASDP II kupitia wadau mbalimbali wa kilimo |
| | | | Kuimarisha usindikaji wa mazao mbalimbali katika ngazi ya kaya ili kuongeza | Kuhamasisha na kutoa elimu ya usindikaji wa mazao ya kilimo na mifugo kwa vikundi 11 vya wakulima katika vijiji 11 ifikapo Desemba | Elimu ya usindikaji wa mazao imetolewa katika vikundi 6 katika vijiji vya Mangawe, | 2,200,000 | Kazi hii imetekelezwa na Halmashauri na ASDP II kupitia wadau mbalimbali wa kilimo |

| | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | thamani na muda wa matumizi na upatikanaji wa chakula kwa ujumla. | 2021 | Luganga, Ismani, Mibikimitali, Ilambilole, na Chamdindi kuhusu umuhimu wa kusindika mazao kabla ya kuyauza ili kuongeza thamani ya zao. | | |
| | | | | Kuanzisha na kuviwezesha vikundi 6 vya usindikaji wa mazao ya kilimo na mifugo katika vijiji 6 ifikapo Desemba 2021 | Vikundi vitatu vimeanzishwa kwa ajili ya kufungua viwanda vidogovidogo vya usindikaji wa mazao ya ufuta kama vile Alizeti na Karanga katika Tarafa ya Isimani | 3,000,000 | Kazi hii imetekelezwa na Halmashauri na ASDP II kupitia wadau mbalimbali wa kilimo |
| | | | Kusimamia utaratibu wa mashindano ya kilimo kinachozingatia kanuni bora za kilimo kati ya vijiji, kata, tarafa, wilaya | Kushindanisha wakulima katika ngazi mbalimbali ikiwa ni vijiji 134 kata 28 na tarafa 6 mara moja kila mwaka na kupata wakulima watakaoshiriki katika | Shughuli za maonyesho ya nane nane zimesitishwa kwa mwaka 2021 | 0 | Kazi kwa msimu wa 2021 haipo |

| | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | na mikoa. | maonyesho ya nanenane kikanda Jijini Mbeya ifikapo Desemba 2021. Pia kuanzisha maonesho ya Nane Nane katika ngazi ya kata | | | |
| | | | Kuimarisha uongozi wa Vyama vya Ushirika na kuvijengea uwezo kujiendesha kwa ufanisi. | Kutoa mafunzo kwa vyama vya ushirika 30 juu ya usimamizi na uendeshaji wake ifikapo Desemba 2021. | Jumla ya vyama 17 vya Ushirika (10 vya SACCOS na 7 vya AMCOS) vilipatiwa mafunzo ya uendeshaji na usimamizi kwa wajumbe wa bodi 119 katika vyama vyote kwa kuzingatia Sheria za vyama vya Ushirika Na 6 ya mwaka 2013. | 2,035,000 | Kazi hii imetekelezwa na Halmashauri kwa kushirikiana na Tume ya maendeleo ya ushirika na IFCU, ASDP II Utekelezaji kwa vyama 13 unaendelea. |
| | | | Kuimarisha shughuli za ukaguzi na usimamizi wa Vyama vya Ushirika nchini. | Kufanya ukaguzi wa mahesabu na uendeshaji wa vyama vya ushirika 38 ifikapo Desemba 2021 | Jumla ya vyama 17 vimekaguliwa zikiwemo SACCOS 9, AMCOS 6, Maziwa 1 na Maduka mawili | 2,050,000 | Kazi hii imetekelezwa na Halmashauri kwa kushirikiana na Halmashauri na Tume ya maendeleo ya ushirika na COASCO |

| | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | *Sekta ya Umwagiliaji* | 34 | Kuendelea kutekeleza umwagiliaji kupitia Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Kilimo kwa kuongeza eneo lenye miundombinu ya umwagiliaji kutoka hekta 326,492 za Juni 2010 hadi hekta 1,000,000 ifikapo mwaka 2015 na hivyo kujitosheleza kwa zao la mpunga. Sekta binafsi itashirikishwa katika uendelezaji na uwekezaji kwenye kilimo cha umwagiliaji. | Kuongeza eneo lenye miundombinu ya umwagiliaji kwa kiwango cha Hekta 23,215 za mpunga na mazao mengine ifikapo Desemba 2021 | Jumla ya hekta 167 za umwagiliaji zimeongezaka baada ya ukarabati wa skimu ya Umwagiliaji Mafuruto kufanyika. | 200,000,000 | Shughuli zimetelezwa kwa ufadhili wa serikali ya Japan kupitia JICA hususani mfuko wa FACF |
| | | | | Kuboresha/kukarabati miundombinu ya umwagiliaji kwa kuongeza idadi ya scheme za umwagiliaji kutoka 25 hadi 35 ifikapo Desemba 2021 | -Umefanyika ukarabati wa miundombinu ya umwagiliaji katika skimu za umwagiliaji za Magozi, Mlenge na Mkombozi ambazo ziliathiriwa na mafuriko ya msimu wa 2019/2020 na kuongeza eneo la umwagiliaji kwa Ha. 1,400 | 20,000,000 | Kazi hii imetekelezwa na Halamshauri ya Wilaya kwa kushirikiana na wananchi |

| | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | Kujenga na kukarabati mabwawa ya kuvuna na kuhifadhi maji ya mvua na mito kwa ajili ya umwagiliaji; | Kukarabati bwawa 1 la kuvuna na kuhifadhi maji ya mvua na mito kwa ajili ya umwagiliaji katika kijiji cha mgama ifikapo Desemba 2021. | Utafutaji wa fedha kwa ajili ya ukarabati wa bwawa la Mgama unaendelea kwa kushirikisha wadau | 0 | |
| | | | Kuhamasisha uanzishaji na uimarishaji wa vikundi vya ushirika wa wafugaji. | Kuimarisha uanzishaji wa vikundi 6 vya ushirika wa wafugaji ifikapo Desemba 2021. | Vikundi 3 vya wafugaji wa maziwa vyenye jumla ya wanachama 17 vilihamasishwa na kujiunga katika Ushirika wa Maziwa uliopo wa **(Iringa Dairy Cooperative Society)** | 2,500,000 | Kazi hii imefanywa na Halmashauri na Tume ya Maendeleo ya Ushirika. |
| 4. | SERA YA UWEZESHAJI WANANCHI KIUCHUMI Kuendelea kutekeleza sera ya uwezeshaji wa wananchi kiuchumi. | 76 | Kuendelea kutekeleza sera ya uwezeshaji wa wananchi kiuchumi kwa kuchukua hatua zifuatazo:- | | | | |
| | | | Kuendeleza utekelezaji wa Mfumo wa | Kutoa mafunzo juu ya kuanzisha mfumo wa stakabadhi | Mafunzo yametolewa kwa wakulima | 600,000 | Kazi hii imetekelezwa na Halmashauri |

| | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | Stakabadhi ya Mazao Ghalani. | ghalani kwa wakulima 7,500 katika vijiji 12 ifikapo Desemba 2021 | wa mpunga katika ghala la Isele na shughuli ya uhifadhi imeanza. | | na ASDP II kupitia wadau mbalimbali wa kilimo pamoja na Tume ya Ushirika |
| | | | Kuhamasisha uanzishwaji wa ushirika wa kuweka na kukopa (SACCOS na VICOBA), wa mazao, ujenzi, uvuvi, biashara na aina nyingine za ushirika ili wananchi wengi zaidi wajiunge na ushirika na wawezeshwe kimtaji kupanua shughuli zao za uzalishaji mali. Serikali izingatie kwa ukamilifu uzoefu ambao umepatikana katika eneo | Kuimarisha SACCOS 28 zilizopo na kuhamasisha wananchi kujiunga na SACCOS katika vijiji 25 ifikapo Desemba 2021 | Jumla ya SACCOS 12 ziliimalishwa kwa kuongeza wanachama 82 katika vyama vyao na kuongeza mtaji wa Hisa kwa kufikia kiasi cha Tsh 1,640,000/= | 1,435,000 | Kazi hii imetekelezwa na Halmashauri na ASDP II kupitia wadau mbalimbali wa kilimo pamoja na Tume ya Ushirika |

| | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | hili la ushirika na iandae wataalam wengi wa ushirika ambao wataajiriwa kuimarisha na kuboresha sekta ya ushirika nchini kote | | | | |
| | | | Kuimarisha usimamizi na matumizi ya fedha za Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake na Vijana katika Halmashauri zote ili uweze kuwanufaisha vijana wengi zaidi kupitia SACCOS zao. | Kutoa mikopo kwa vikundi 10 na kuuendelea kuwahamasisha vijana katika vjiji kujiunga katika vikundi vya uzalishaji mali ili waweze kupata mikopo kupitia SACCOS ifikapo Desemba 2021 . | Halmashauri imeanzisha SACCOS moja ya Vijana yenye jumla ya wanachama 106, Me 86 na Ke 20.Lengo ikiwa ni kuwawezesha vijana kupata mikopo yenye riba nafuu pamoja kuanzisha shughuli za kiuchumi za pamoja | 1,050,000 | Kazi hii imetekelezwa na Halmashauri, Tume ya maendeleo ya Ushirika.Heifer na Restless Development |
| | | | Kushirikiana na wadau wengine katika kuimarisha | Kuhamasisha vikundi 2 vya vijana kujiunga na SACCOS na kuendelea kutoa elimu ya umuhimu | Jumla ya Vikundi 13 vilihamasishwa na kuanzisha Ushirika wa | 1,500,000 | Kazi hii imetekelezwa na Halmashauri na Tume ya maendeleo ya |

| | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | vyama vya vijana vya ushirika wa akiba na Mikopo (SACCOS) ili viweze kutoa mikopo yenye masharti nafuu kwa vijana. Umuhimu wa kulipa mikopo kwa wakati utasisitizwa. | wa kulipa mikopo kwa wakati ifikapo Desemba 2021. | vijana wa Iringa(Iringa Youth Saccos) wenye jumla ya wanachama 106 Me 86 na Ke 20 na kupatiwa usajiri wa mpito kwa mujibu wa Sheria ya Ushirika Na 6 ya mwaka 2013. | | ushirika.Restless na Heifer |
| | **JUMLA NDOGO** | | | | | **332,086,500** | |

**SEKTA YA MIFUGO NA UVUVI**

| NA | SEKTA/SERA | IBARA | MALENGO/ MAELEKEZO YA ILANI | MPANGO WA MWAKA | UTEKELEZAJI | GHARAMA | MAELEZO |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | *Mapinduzi ya Mifugo* | 38 | Kuelimisha wafugaji uwiano kati ya idadi ya mifugo na kutenga maeneo Kutenga, kupima na kumilikisha maeneo ya shughuli za ufugaji kwa | Kuelimisha wafugaji uwiano kati ya idadi ya mifugo na maeneo katika vijiji 5 pamoja uboreshaji wa nyanda za malisho ifikapo Desemba 2021 | Halmashauri imetoa elimu kwa wafugaji 2,179 juu ya kuboresha uwiano wa mifugo na maeneo ya malisho kwa lengo la kuongeza tija sambamba na | 500,000 | Fedha hizi zimetolewa na wadau wa urasimishaji ardhi wa LTA USAID |

| | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | wafugaji katika halmashauri zote nchini | | uboreshaji nyanda za malisho katika vijiji 8 vya Mbugani, Mboliboli, Izazi, Kibena, Lumuli, Ibangamoyo, Kikombwe, Kaning'ombe na Sadani | | |
| | | | | Kutenga, kupima na kumilikisha maeneo ya malisho hekta 20 kwa vijiji 5 ifikapo Desemba 2021 | Halmashauri Imetenga, kupima na kumilikisha maeneo ya malisho hekta 1,402.43 kwa ufadhili wa Mradi wa urasimishaji ardhi vijijini LTA katika vijiji 6 vya Kibena, Lumuli, Ibangamoyo, Kikombwe, Kaning'ombe na Sadani | 3,000,000 | Fedha zimetolewa na mradi wa kurasimisha ardhi vijijini LTA USAID |

| | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Sekta3 ya mifugo ni miongoni mwa sekta muhimu katika ukuaji wa uchumi Kutokana na umuhimu huo, ni dhahiri kuwa ipo haja ya kuendelea kuimarisha ufugaji wa kisasa na kuchakata/kusarifu bidhaa za mifugo kwa ajili ya mahitaji ya ndani, ikiwemo ya lishe bora, na usafirishaji nje. | | | | | 0 | |
| | | | Kuanzisha mashamba darasa(FFS) na usambazaji wa teknolojia za mifugo ili kuwa na malisho ya kutosha | Kuanzisha mashamba darasa 5 (FFS) sambamba na usambazaji wa teknolojia za mifugo ili kuongeza malisho kwa mifugo ifikapo Desemba 2021 | Halmashauri imeanzisha mashamba darasa mapya ya malisho katika vijiji 4 vya Ifunda, Tosamaganga, Mangalali na | 0 | Mapato ya ndani |

| | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | Nzihi kwa lengo la kuboresha lishe kwa mifugo na kipato. | | |
| | | | Serikali isimamie kwa ufanisi mkubwa mradi wa kuboresha koosafu ya mifugo kama hatua ya kueneza ufugaji wa kisasa wenye tija kubwa. | Kuhamasisha mradi wa kuboresha koosafu za mifugo kwa kutumia madume bora na uhimilishaji kwa vijiji 4 ifikapo Desemba 2021 | Halmashauri kwa kushirikiana na wadau wa ABEA na Heifer International imeendelea kuboresha koosafu kwa kutumia madume bora 3 kijiji cha Ilolompya na kwa njia ya uhimilishaji vijiji vya Kiponzelo, Ifunda, Kaning,ombe, Lyamgungwe, Lwato na Mgama ambapo ng’ombe 201 walihimilishwa. | 1,300,000 | - |
| | | | Kuendeleza elimu kwa Wafugaji ili wajue kuwa mifugo waliyonayo ni | Kutoa mafunzo kwa wafugaji juu ya ufugaji wenye tija pamoja na athari za kutohamahama katika vijiji 5 ifikapo | Halmashauri imetoa mafunzo ya ufugaji bora wenye tija na usio wa | 500,000 | Shughuli hii imefanyika kwa kushirikiana na wadau na azaki za kimaendeleo ya mifugo |

| | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | mali inayoweza kuvunwa katika umri na uzito muafaka unaokidhi mahitaji ya soko, ili kuwaondolea umaskini wao badala ya kuridhika na wingi wa mifugo iliyo duni na maisha ya kuhamahama. | Desemba 2021 | kuhamahama kwa wafugaji 795 wa vijiji 4 vya Mboliboli, Kitisi, Mbugani, Makadupa na Ikengeza. | | |
| | | | Kufufua na kujenga majosho na malambo mapya kwa ajili ya mifugo na kuhimiza uogeshaji endelevu | Kujenga na kukarabati majosho 2, machinjio ndogo 1, kisima kirefu 1, lambo 1 na mabirika 3 kwa ajili ya mifugo na kuhimiza uogeshaji endelevu katika vijiji 6 ifikapo Desemba 2021 | Halmashauri imefanya uhakiki wa majosho 21 yenye kuhitaji ukarabati na majosho 2 yamekarabatiwa katika vijiji 2 vya Nyakavangala na Wasa. Pia umefanyika ufuatiliaji wa ujenzi wa kisima kirefu 1 katika kijiji cha Usolanga kilichofikia | 59,350,000 | Fedha hizi zinatolewa na Wizara ya Mifugo na Uvuvi kitengo cha uendelezaji majosho nchini |

| | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | hatua ya umaliziaji na ujenzi wa birika 1. | | |
| | | | Kuimarisha huduma za ugani na mafunzo ya wataalamu na wafugaji. | Kutoa mafunzo ya ukaguzi wa nyama na ngozi, ufugaji bora wa mifugo wenye tija kwa maafisa ugani 10, wachinjaji 6 na wafugaji 6 ifikapo Desemba 2021 | Mafunzo na ukaguzi wa wachunaji na ukaguzi wa nyama yametolewa kwa wataalam 6 na wachunaji 12 ili kuimarisha ubora wa ngozi katika machinjio ya ya Igingilanyi | 500,000 | - |
| | | | Kuimarisha huduma za afya ya mifugo kwa kudhibiti magonjwa ya mifugo hasa ya milipuko na uanzishwaji wa Maeneo Huru kwa Magonjwa ya Mifugo. | Kuendelea kutoa chanjo na tiba mbalimbali kwa ng'ombe 95,097, Mbuzi 78,000, kondoo 6,715, Punda 5,749, Nguruwe 15,281 na kuku 728,387 ili kudhibiti magonjwa ya mifugo ifikapo Desemba 2021. | Halmashauri imetoa chanjo ya Homa ya mapafu ya ng'ombe (CBPP) ng'ombe 36,780 na chanjo ya Mdondo na Mahepe kwa kuku 569,421 katika vijiji na kata kila baada ya miezi 3. Aidha tiba mbalimbali za | 1,500,000 | - |

| | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | mifugo zimetolewa kwa ng'ombe 56,006, mbuzi 33,871, kondoo 2,163, punda 498, nguruwe 8,951 na kuku 342,091 | | |
| | | | Kuhamasisha uanzishaji na uimarishaji wa vikundi vya ushirika wa wafugaji. | Kuimarisha uanzishaji wa vikundi 2 vya ushirika wa wafugaji katika kata 2 za Ifunda na Nzihi. | Halmashauri imeendelea kuimarisha Vikundi 2 vya ushirika wa wafugaji ng'ombe wa maziwa Ifunda (IDCO) na kikundi cha wafugaji Nzihi kwa kutoa mafunzo kwa wafugaji 56 ili kuwajengea uwezo ili kusimamia na kujiendesha kwa faida | 610,000 | - |
| | Tanzania ina fursa maalum ya kuendeleza uchumi wake kupitia rasilimali | 43 | | | | 0 | - |

| | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | zilizo katika bahari, maziwa, mito na mabwawa kama vile uvuvi na ufugaji wa samaki na mazao mengine | | | | | | |
| | | (p) | Kushirikiana na wadau wa ufugaji samaki ili kuongeza uzalishaji wa samaki kwa kujenga mabwawa ya kufugia samaki | Kutoa eilimu ya ufugaji wa samaki kwa wafugaji 35 na uchimbaji wa mabwawa ya ufugaji wa samaki 15 ifikapo Disemba, 2021 | Halmashauri imeendelea kutoa elimu ya ufugaji bora wa samaki katika mabwawa ya kuchimbwa kwa wafuhaji 59 walioko katika vijiji vya Ikuvilo, Igangidung'u, Mgama, kihanga Kiponzelo, Wasa, Lyamgungwe na Kiwere sambamba na kuchimba mabwawa 9 bora na kuyapanda samaki bora aina ya Perege, | 1,400,000 | Elimu ya ufugaji bora wa samaki imefadhiliwa mradi wa shirika lisilo la kiserikali la World Vision kwa kumsafirisha na kumkimu mkufunzi |

| | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | sato na kambalen katika vijiji 6 vya Ikuvilo, Kihanga, Igangidung'u, Mgama, Wasa na Tangangozi | | |
| | | (i) | Kuanzisha na kuimarisha vikundi vya ulinzi shirikishi vya kudhibiti uvuvi haramu | Kuimarisha vikundi 10 vya kudhibiti uvuvi haramu katika bwawa la Mtera ifikapo Desemba, 2021 | Halmashauri imeimarisha vikundi 7 vya ulinzi shirikishi katika bwawa la Mtera kwa kuwajengea uwezo wa kupambana na uvuvi haramu pamoja na matumizi ya zana za uvuvi zinazoharibu mazalia ya samaki na uharibifu wa mazingira katika kata za Izazi na Migoli | 450,000 | Halmashauri imegaramia mafuta ya boti kwa ajili ya shughuli za kudhibiti uvuvi haramu |
| | **JUMLA NDOGO MIFUGO NA UVUVI** | | | | | **68,110,000** | |

## SEKTA YA VIWANDA NA BIASHARA

| NA | SEKTA/SERA | IBARA | MALENGO/MAELEZO YA ILANI | MPANGO WA MWAKA | UTEKELEZAJI | GHARAMA | MAELEZO |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | *(i) Viwanda:-* Chama Cha Mapinduzi kinatambua kuwa sekta ya viwanda ni nguzo muhimu katika kukuza uchumi wa nchi, kukuza pato la mwananchi, | 49 | .Kujenga na kuimarisha ujuzi katika biashara na kuweka msukumo zaidi katika kutumia fursa za masoko. | Kuendelea kuwawezesha sekta binafsi 10 kushiriki katika maonyesho ya Biashara ifikapo Desemba 2021. | Sekta binafsi 11 zimeshiriki katika maonyesho ya bidhaa za viwanda vya ndani chuo kikuu cha Mkwawa Iringa 2021. | 300,000 | |
| | kupunguza umasikini na kuongeza uwezo wa Taifa kujitegemea | | Kuandaa taarifa kuhusu fursa za uwekezaji katika miradi ya maendeleo ya viwanda nchini. Kujenga na kuimarisha ujuzi katika biashara na kuweka msukumo zaidi katika kutumia fursa za masoko | Kutangaza wasifu wa uwekezaji (investment Profiles) kwa wadau mbalimbali ili waelewe fursa za uwekezaji zilizopo katika Wilaya kupitia mikutano 2 ya uhamasishaji. ifikapo Desemba 2021 | Umefanyika Mkutano 1 kwa ajili ya kutangaza wasifu wa uwekezaji (investment Profile) kwa wadau mbalimbali ili waelewe fursa za uwekezaji zilizopo | 600,000 | |

| | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | | | |
| | *(ii) Viwanda Vidogo* | 50 | Kuongeza mchango wa viwanda vidogo na biashara ndogo (SMEs) katika pato la Taifa kutoka asilimia 33 ya GDP hivi sasa kufikia asilimia 40 mwaka 2021. | Kuhamasisha matumizi ya zana na teknolojia bora kwa wafanya biashara wadogo 120 ili kuzalisha bidhaa bora kwa gharama nafuu ifikapo Desemba 2021 | Vijana 60 wameshapatiwa mafunzo kutoka shirika la SIDO na kununua mashine za teknolojia rahisi. Aidha viwanda vidogo 12 vikiwemo vya kuongeza thamani mazao ya nafaka 7, samani 4 na mbao 1. vimeanzishwa katika Halmashauri | 280,000 | |
| | | | Kuendeleza miundombinu ya viwanda vidogo na biashara ndogo. | Kutenga na kuyaendeleza maeneo kwa ajili ya viwanda vidogo 4 na Biashara ndogo | Maeneo ya biashara ndogondogo katika eneo la ujenzi wa stendi ya mabasi Migoli | 10,000,000 | |

| | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | 8 ifikapo Desemba 2021 | na eneo la burudani Igingilanyi yanayotengwa kwa ajili ya wafanyabiashara wadogowadogo | | |
| | | 51 | Kutoa mafunzo ya kuwajengea uwezo wajasiriamali kuhusu mbinu za kuyafikia masoko ya nje. | Kutoa mafunzo ya kuwajengea uwezo vikundi 4 vya wajasiriamali kuhusu mbinu za kuyafikia masoko ya nje ifikapo Desemba 2021. | Vikundi 2 vya wajasiriamali vya Tanangozi na Mbuyuni vimejengewa uwezo kuhusu mbinu za kuyafikia masoko ya nje | 120,000 | |
| | *(iv) Mapinduzi ya Kilimo* | | Kuratibu na kuhamasisha ushiriki wa wajasiriamali wa Tanzania katika maonesho ya biashara ya kimataifa ndani na nje ya nchi. | Kuendelea kuviunganisha vikundi 18 vya wajasiariamali na mitandao mbalimbali ya masoko ifikapo Desemba 2021 | Vikundi 5 vya wajasiria mali vimeunganishwa na mitandao mbalimbali ya masoko | 260,000 | |
| | *(v)* | 52 | Kufanya utafiti wa masoko na bei ili kupanua wigo wa mahitaji ya masoko ya bidhaa zetu. | Kuendelea kuviunganisha vikundi 9 vya wajasiariamali na mitandao mbalimbali ya masoko ifikapo Desemba 2021. | Vikundi 5 vya wajasiria mali vya Tagamenda, Mgama, Tanangozi, Luganga, na Mbuyuni, vimeunganishwa na mitandao mbalimbali ya | 120,000 | |

| | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | masoko | | |
| C | *(i) Masoko* | 53 | Kuendeleza biashara ya ndani ikiwa ni pamoja na kujenga dhana ya kutumia bidhaa zilizozalishwa Tanzania (NUNUA BIDHAA ZA TANZANIA). | Kuendelea kuhamasisha jamii kutumia bidhaa zinazozalishwa ndani katika vijiji 134 ifikapo Desemba 2021 | Umefanyika uhamasishaji kwa jamii kutumia bidhaa zinazozalishwa ndani katika vijiji 60 | 80,000 | |
| | | | Kuendeleza na kuboresha mfumo wa ukusanyaji, uhifadhi, uchambuzi na usambazaji wa taarifa za masoko. | Kuhakikisha uwepo na matumizi sahihi ya mbao za matangazo katika vijiji 48 ifikapo Desemba 2021 | Vijiji 22 kati ya Vijiji 134 vina mbao za matangazo na zinatumika | 60,000 | Mbao za matangazo zinatumika |
| | | | Kuboresha mazingira ya kufanya biashara kwa kutekeleza Sheria ya Usajili wa Shughuli za Biashara (BRELA). | Kuendelea kusajili Biashara ambazo hazijasajiliwa katika vijiji 91 ifikapo Desemba 2021 | Biashara ambazo zilikuwa bado hazijasajiliwa zimesajiliwa katika Vijiji 61. Aidha Biashara mpya 203 zimesajiliwa katika utoaji wa huduma ya fedha kwa mtandao | 360,000 | |
| **JUMLA NDOGO** | | | | | | **11,880,000** | |

**SEKTA YA ARDHI**

| NA | SEKTA/SERA | IBARA | MALENGO/ MAELEKEZO YA ILANI | MPANGO WA MWAKA | UTEKELEZAJI | GHARAMA | MAELEZO |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **NA** | **SEKTA/SERA** Sekta ya miundo mbinu na huduma za kiuchumi<br><br>i. ARDHI Ardhi, imekuwa muhimu katika kuziwezesha sekta nyingine kuzalisha kikamilifu hususan sekta za uzalishaji kama vile kilimo, mifugo, uvuvi ikiwa ni pamoja na maeneo ya ardhi kwa ajili ya ujenzi wa viwanda. | **IBARA** 59 (a) | **MAELEZO YA ILANI** | **MPANGO WA MWAKA** | | | |
| | | | Kwa kushirikiana na Halmashauri za Wilaya na Miji, kukamilisha kazi ya upimaji wa mipaka ya Vijiji vipya na kupanga mipango ya Matumizi Bora ya Ardhi. Vile vile kuwahamasisha wananchi kuchangia upimaji wa mashamba yao na kuwapatia hatimiliki za Kimila, pamoja na kujenga Masjala za ardhi katika ngazi za Wilaya na Vijiji. | Kuandaa mpango wa matumizi bora ya ardhi katika vijiji 3 vya Isele , Makadupa na Mikong'wi ifikapo Desemba 2021 | Hakuna mpango wa matumizi bora ya ardhi ulioandaliwa katika kipindi hiki cha taarifa | 0 | Kazi hii itafanyika mwaka wa fedha ujao |
| | | | | Kupima mipaka katika vijiji vipya 3 vya Uhominyi, Ivangwa na Mikong'wi ifikapo Desemba 2021 | Jumla ya vijiji viwili vya lwato na Ilandutwa vimepimwa pamoja na marekebisho ya mipaka ya vijiji vya Kibena, muwimbi, mfukulembe, udumka, mibikimitali, | 0 | Upimaji umefanyika kuruhusu zoezi la utoaji hati za kimila unaofadhiliwa na LTA |
| | | | | Kutoa hati miliki 350 za kimila katika Tarafa za Mlolo, Kiponzero, Idodi na Isimani ifikapo Desemba 2021 | Jumla ya hatimiliki 7,150 za kimila zimetolewa katika vijiji vya Msuluti, Kihanga, Sadani na Kaning'ombe | 0 | Shughuli hii imetekelezwa kwa kushirikiana na Mradi wa LTA |
| | | | | Kuanzisha masijala za ardhi katika vijiji 2 vya | Jumla ya Vijiji 36 kati ya Vijiji 134 vina masjala za | 0 | Shughuli hii imetekelezwa kwa |

| | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | Lupembewasenga na Matembo ifikapo Desemba 2021 | ardhi zilizokamilika | | kushirikiana na Mradi wa LTA |
| | | 59 (i) | Kutoa elimu kwa umma juu ya Sheria za Ardhi, Sheria ya Mipango Miji, Sheria ya Mipango ya Matumizi Bora ya Ardhi na Sheria zingine zinazohusiana na utawala wa Ardhi | Kuendelea kutoa elimu kwa umma juu ya Sheria za Ardhi, Sheria ya Mipangomiji, Sheria ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi na sheria zingine katika vijiji 3 vya Wangama, Uhominyi na Ivangwa ifikapo Desemba 2021 | Sheria za ardhi na Sheria ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi zimetolewa katika vijiji vya Msuluti, Kihanga, Sadani, Mfyome, Mibikimitali, Ng'enza na kaning'ombe | 0 | Shughuli hii imetekelezwa kwa kushirikiana na Mradi wa LTA |
| | ii. NYUMBA | 60 (a) | Kuhakikisha kwamba ujenzi wa nyumba na majengo yanatumiwa na umma unazingatia mahitaji maalum hususan ya watu wenye ulemavu. | Kuendelea kuzingatia mahitaji maalumu ya walemavu katika ujenzi wa majengo ya Umma katika miji midogo ya Ihemi, Ugwachanya na Kalenga ifikapo Desemba 2021 | Ujenzi wa majengo ya Umma katika miji midogo ya Ihemi, Ugwachanya na Kalenga imezingatia mahitaji maalumu ya walemavu | 0 | |
| | iii MIPANGOMIJI | 60 (b) | Kushirikiana na Halmashauri za Miji na Majiji kutekeleza Mpango wa kuboresha makazi yaliyojengwa | Kuendelea na zoezi la upimaji wa viwanja katika miji midogo 6 ya Kalenga, Isakalilo, Ugwachanya, Tagamenda, | Jumla ya viwanja 663 vimerasimishwa katika maeneo ya kimpango ya Isakalilo. | | Urasimishaji umefanywa kwa fedha za michango ya wananchi |

| | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
